




Hamisi Abahatika

Adelheid Marie Bwire

Rob Owen

Kiswahili





Siku moja Hamisi na babake walienda sokoni kununua sare ya shule.



Hamisi akamwona kijana mwingine amevalia shati la kijani kibichi. "Anaonekana nadhifu sana," Hamisi aliwaza.



"Shati lile lapendeza sana," Hamisi alimwambia babake.



Hamisi aliendelea kusema, "Tafadhali baba, ninunulie shati la kijani kibichi."



"Hamisi, leo nitaweza kununua sare ya shule pekee." Baba alisema.



"Sina pesa za ziada za kukununulia shati kama hilo." Baba akaeleza.



Baada ya kulipia sare, baba alitambua kuwa alikuwana pesa zilizobaki. Angeweza kumnunulia Hamisi shati la kijani kibichi!



Hamisi alifurahi sana. Alikimbia kwenda kujichagulia shati la kijani kibichi.

You are free to download, copy, translate or adapt this story
and use the illustrations as long as you attribute in the
following way: Adelheid Marie Bwire Author - Adelheid Marie
Bwire

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First sentences © African Storybook Initiative and
Molteno Institute 2014

Creative Commons: Attribution 3.0

Source www.africanstorybook.org

